

HALMASHAURI YA WILAYA UYUI



TANGAZO LA KUPANGISHA MAENEO YA KUJENGA VIBANDA VYA BIASHARA STENDI YA MAGARI ISIKIZYA

MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURIYA WILAYA UYUI ANAKARIBISHA WAPANGAJI AMBAO WATAJENGA VIBANDA, WATAFANYA BIASHARA NA MARA BAADA YA KURUDISHA GHARAMA ZAO WATAVIKABIDHI KWA HALMASHAURI AMA KUENDELEA KUPANGA KWA MKATABA

FOMU ZINATOLEWA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI KWA GHARAMA YA TSHS. 20,000, VILEVILE KILA MPANGAJI ANATAKIWA KUCHANGIA TSHS. 150,000 KWA AJILI YA UENDELEZAJI WA STENDI

**(USOGEZAJI WA UMEME, USOGEZAJI WA MAJI, KUTENGENEZA BARABARA, KUJENGA KIBANDA CHA MTOZA USHURU NA CHA ASKARI, KUJENGA BANDA LA ABIRIA NA KUSAFISHA ENEO LA STENDI)
AIDHA UTAKAPOFIKA HALMASHAURI UTAPATIWA:**

- **GHARAMA KAMILI ZA UJENZI WA KIBANDA**
- **UTARATIBU WA KULIPIA**
- **MUDA WA KUANZA BIASHARA BILA KULIPIA (GRACE PERIOD)**
- **MKATABA NA MASHARTI YAKE**

❖ NAFASI ZIPO 150 TU, WATAKAOWAHI NDIO WATAKAOPATA

KAZI YA UJENZI INATAKIWA IFANYIKE NDANI YA MIEZI MITATU (3) BAADA YA KULIPIA GHARAMA ZILIZOTAJWA

YEYOTE ATAKAYETAKA KUPANGA ENEO AFIKE OFISINI KWA MKURUGENZI ILI KUPEWA UFAFANUZI ZAIDI

MAOMBI YANAPOKELEWA KUANZIA TAREHE 10 JUNI 2021 NA MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 30 JUNI SAA 9.30 MCHANA

KARIBUNI SANA

**HEMED S. MAGARO
MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA - UYUI
TAREHE 10JUNI, 2021**